**HOTUBA YA MHE. JAJI (RUFAA) JACOBS C. M. MWAMBEGELE MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI, WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO KWA WATENDAJI WA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA, JIMBO NA KATA,YANAYOFANYIKA MKOANI IRINGA TAREHE 24 JANUARI HADI TAREHE 26 JANUARI, 2026**

- **Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti;**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Tume;**
- **Ndugu Mkurugenzi wa Uchaguzi;**
- **Ndugu Mwenyekiti wa Mafunzo;**
- **Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa wa Mikoa ya Ruvuma na Songwe;**
- **Wasimamizi wa Uchaguzi;**
- **Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na Kata;**
- **Maafisa Uchaguzi:**
- **Maafisa Ununuzi;**
- **Wahasibu:**
- **Watendaji wa Tume;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Ndugu Washiriki,**

1. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana siku hii ya leo **tarehe 24 Januari, 2026** hapa Mkoani Iringa tukiwa wazima wa afya, na niwatakie kheri ya mwaka mpya 2026.

2. Aidha, niwapongeze kwa uteuzi wenu ambao umezingatia masharti ya kifungu cha 6 (1), (2) na (5) na kifungu cha 8 (1) na (2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024. Uteuzi wenu pamoja na mambo mengine umezingatia weledi, utendaji kazi mzuri, uzoefu wenu katika masuala ya uchaguzi na uaminifu wenu katika utekelezaji wa majukumu mtakayokabidhiwa na Tume. **HONGERENI.**

3. Ninawasisitiza kuheshimu viapo vyenu kwa nafasi mlizoteuliwa, tekelezeni majukumu yenu kwa kuzingatia Katiba ya Nchi, Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake, Kanuni za Maadili ya Uchaguzi na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na yatakayotolewa na Tume katika kipindi hiki cha uchaguzi.

**Ndugu Washiriki,**

4. Kama mnavyofahamu kwa mujibu wa ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, jukumu la kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na wabunge wa Jamhuri ya Muungano na madiwani kwa Tanzania Bara ni la Tume, lakini matakwa ya kisheria yanaelekeza wawepo waratibu wa uchaguzi, wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi

wasaidizi wa uchaguzi wa jimbo na kata kwa ajili ya kuendesha uchaguzi, ndiyo sababu wote mliopo hapa mmeteuliwa kutekeleza jukumu hilo kwa niaba ya Tume.

**Ndugu Washiriki,**

5. Kwa niaba ya Tume natoa shukrani za dhati kwenu nyote kwa kuitikia wito wetu na kufika hapa kwa ajili ya kushiriki mafunzo yatakayotolewa kwa muda wa siku tatu kuanzia leo tarehe 24 Januari, 2025 hadi tarehe 26 Januari, 2026.

6. Mafunzo haya yanahusisha waratibu wa uchaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na Kata, maafisa uchaguzi, maafisa ununuzi na Wahasibu. Lengo likiwa ni kukumbushana masuala muhimu kuhusiana na usimamizi, uratibu na uendeshaji wa uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga.

7. Katika mafunzo haya, jumla ya mada kumi zitawasilishwa ambapo tutapata fursa ya kubadilishana uzoefu na kujadiliana namna ya kufanikisha uchaguzi katika maeneo yetu. Aidha, tutajadiliana namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika hatua zote za uchaguzi.

8. Kwa wale mnaosimamia uchaguzi kwa mara ya kwanza, ni mategemeo yangu kuwa mtajifunza kwa haraka na mtapata uzoefu kupitia majadiliano ya pamoja. Vilevile, kwa upande wa wale

wazoefu, mtatumia fursa hii kujiongezea maarifa mapya na kubadilishana uzoefu na washiriki wengine.

9. Ni matarajio ya Tume kuwa, baada ya mafunzo haya kila mmoja wenu atapata elimu na ujuzi wa kutosha utakaomuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi

**Ndugu Washiriki;**

10. Uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu mbalimbali za kisheria ambazo hupaswa kufuatwa na kuzingatiwa kwani hatua na taratibu hizo ndio msingi wa uchaguzi kuwa mzuri na wenye ufanisi, hivyo kupunguza kama sio kuondoa kabisa malalamiko au vurugu wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

11. Nachukua nafasi hii kuwaasa kuwa, pamoja na uzoefu ambao baadhi yenu mnao katika uendeshaji wa uchaguzi, mhakikishe mnazingatia maelekezo mtakayopewa na Tume badala ya kufanya kazi kwa mazoea. Kwani kila uchaguzi unatofautiana na uchaguzi mwingine.

**Ndugu Washiriki;**

12. Wakati wote wa mchakato wa uchaguzi huu, ni vema mkavishirikisha kwa karibu vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili na wadau wengine wa uchaguzi katika maeneo yenu kuhusu masuala ya kiuchaguzi ambayo wanastahili kushirikishwa kwani jambo hilo litawarahisishia utekelezaji wa majukumu yenu.

13. Ni muhimu kwenu pia, kuhakikisha mnayatambua na kuyajua vyema maeneo ambayo uchaguzi utaendeshwa ikiwemo miundombinu ya kufika katika vituo vya kupigia kura.

**Ndugu Washiriki;**

14. Pamoja na mambo niliyobainisha hapo awali, napenda kuwasisitiza masuala muhimu yafuatayo:-

    i. Kufanya utambuzi wa vituo vya kupigia kura mapema ili kubaini mahitaji maalum ya vituo husika na kuhakikisha kunakuwa na mpangilio mzuri ambao utaruhusu uchaguzi kufanyika kwa utulivu na amani.

    ii. Kuhakikisha mnaajiri watendaji wa vituo wenye weledi, wanaojitambua na kuachana na upendeleo kwa ndugu na jamaa ambao hawana sifa za kufanya shughuli za uchaguzi.

    iii. Kuhakiki vifaa vya uchaguzi mnavyopokea kutoka Tume na kuhakikisha kila mkuu wa kituo anapata vifaa vyote vya uchaguzi vinavyohitajika mapema.

    iv. Kuvipatia vyama vya siasa orodha ya vituo vya kupigia kura ili kuviwezesha kupanga mawakala.

    v. Kuhakikisha siku ya uchaguzi mnaweka utaratibu utakaowezesha kila kituo cha kupigia kura kufunguliwa saa 1:00 asubuhi.

vi. Kufanya mawasiliano na Tume pale ambapo ushauri utahitajika kuhusiana na masuala ya uchaguzi.

**Ndugu Washiriki;**

15. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, niwaombe mzingatie mafunzo mtakayopewa na mtoe uzoefu wa usimamizi wenu wa siku za nyuma ili iwe ni somo kwetu sote katika utekelezaji wa jukumu lililo mbele yetu.

16. Baada ya maelezo haya, ninawatakia mafunzo mema na kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Peramiho na Udiwani katika Kata ya Shiwinga.

17. Nasasa napenda kutamka kwamba, mafunzo haya ya siku tatu yamefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**